# The Anti-Racism Policy Observatory

Scotland itakuwa na muundo mpya - Utafiti - kuishawishi Serikali ya Scotland pamoja na mashirika mengine ya umma kuwajibika na kujitolea kupinga ubaguzi wa rangi. Utafiti huu utahusisha wataalamu wa ndani, kitaifa na kimataifa ili kujua jinsi gani ubaguzi wa rangi unavyofanyika. Utafiti huu utasaidia Serikali ya Scotland kutunga sera madhubuti na endelevu ili ziweze kutumika kupinga ubaguzi wa rangi. Ili kuhakikisha kuwa vitendo vya kupinga ubaguzi wa rangi nchini Scotland vinawasaidia waathirika wa ubaguzi wa rangi. Tungependa kujua maoni yako.



## Kwa nini tunafanya jitihada hizi sasa hivi?

Janga la UVIKO-19 (COVID-19) limefichua ubaguzi wa rangi katika kiwango cha kimataifa. Hivyo Serikali ya Scotland imeongeza dhamira yake ya kushughulikia ubaguzi wa rangi, haswa katika afya.

Ifikapo 2030, Serikali ya Scotland imejitolea kujenga Scotland yenye kufuata misingi ya haki “ambapo kila mtu anaweza kujisikia yuko nyumbani”[1]. Tunahitaji kutumia na kuendeleza kasi hii, na kutambua kuwa Utafiti huu ni hatua muhimu ya kufuatilia na kutekeleza azma yetu.

## Ni nini kimetokea hapo awali na kwa nini hajawezekana kutekelezwa?

Zaidi ya miaka 20 Kumekuwa na sera 39 zinazohusiana na usawa wa rangi nchini Scotland, pamoja na ahadi, na vitendo 817[2]. Pamoja na hivyo, uboreshaji na ufuatiliaji bado ni mdogo sana.


---

1 https://www.gov.scot/publications/fairer-scotland-action-plan/

2 https://www.gov.scot/publications/crer-anti-racist-policy-making-scotland-review-summary/

Mchoro huu uliyoandaliwa hivi karibuni na Coalition for Racial Equality and Rights (CRER) umeonyesha kuwa kuna mzunguko hatari ambao ndio unazuia juhudi za kupambana na ubaguzi wa rangi.

1. Mpango mpya wa “usawa wa Rangi” unapotangazwa kwa mara ya kwanza, husikika kwa shauku kubwa, lakini mwisho wake unakuwa na utekelezaji mdogo sana.
2. Jamii hazielezwi ni nini kilichofanyika kutokana na maoni yao na mara nyingi hawashirikishwi katika kufanya maamuzi.
3. Hivyo, zinapozinduliwa sera mpya huwa hazifanikiwi, kwa sababu ya kutochukuliwa hatua sahihi.



Hakuna anaewajibika kwa kushindwa kutekeleza sera zinazopinga ubaguzi na vile vile kuna ukosefu wa mwendelezo wa utungaji sera, huku vipaumbele vya kisiasa vikiwa vinaendelea kubadilika.

# Vipi UTAFITI huu utakuwa tofauti?

Ili kuunda mabadiliko ya kweli na ya muda mrefu kwa jamii zilizoathiriwa na ubaguzi wa rangi, Utafiti huu utafanya yafuatayo:

1. **Kupinga ubaguzi wa rangi:** Ni lazima tupinge michakato ambayo ubaguzi wa rangi umepachikwa na kuimarishwa katika mifumo ya taasisi zetu (mfano mashirika, huduma za umma zikiwemo shule na NHS, na serikali ya Scotland).
2. **Kuongozwa na jamii yenyewe:** Sera zinazoundwa kwa jina la jamii zilizoathiriwa na ubaguzi wa rangi zinapaswa kuongozwa na jamii hizo.
3. **Kukuza uwajibikaji kwa jamii:** Serikali inapaswa kufuatilia kile ambacho tayari kimetokea, kufuatilia utekelezaji wa sera zinazopinga ubaguzi wa rangi, na kufahamisha jamii zilizoathiriwa na ubaguzi wa rangi kuhusu matokeo yaliyopatikana.
4. **Kulinda jamii zenye kubaguliwa:** Sehemu salama zinapaswa kuundwa kwa jamii zilizoathiriwa na ubaguzi ili kuimarisha sera za kupinga ubaguzi wa rangi.

# Utafiti huu utafanya nini?

Kazi zifuatazo zimependekezwa kwa ajili ya Utafiti huu. Hata hivyo, hii ni kazi endelevu, vile vile tungependa kupata maoni yako kuhusu hili. Mchakato huu unahusisha mfumo-shirikishi, ambao ni kubuni Utafiti utakaohusisha watu, kwahiyo matokeo ya Utafiti huu yanaweza kuwa tofauti na mapendekezo yaliyoainishwa hapa:

1. **TASWIRA NA ALAMA:** Kufuatilia na kuendeleza kazi zote za ubaguzi wa rangi na kuhakikisha tunapinga ubaguzi wa rangi. Muundo huu ambao unapatikana kwa uwazi utajumuisha kazi zinazofanyika kuhusu afya, pamoja na mambo yote yanayoiathiri jamii kiuchumi, kihistoria, kitamaduni na kisiasa
2. **UCHAMBUZI** wa takwimu kati ya ubaguzi wa rangi na upingaji wa ubaguzi wa rangi kwenye sekta ya umma na kibinafsi.
   - Utafiti huu utaimarisha matumizi mazuri ya takwimu zilizopatikana ili kuboresha upingaji wa ubaguzi wa rangi.
3. **KUHAKIKISHA SERIKALI YA SCOTTLAND INAWAJIBIKA KUPINGA UBAGUZI WA RANGI KATIKA SEKTA ZA UMMA.** Kwa mfano,
   - Taasisi zinapaswa kuandaa hatua madhubuti za kufuatilia njia zinazotolewa kupinga vitendo vya ubaguzi wa rangi
   - Taasisi zinapaswa kutathmini mapungufu ya kitakwimu juu ya ubaguzi wa rangi, matokeo ya mapungufu haya na jinsi yanavyoweza kuondolewa.
4. **KUENDELEZA USHIRIKIANO** kati ya taasisi na watu walioathiriwa vibaya na ubaguzi wa rangi.
5. **KUENDELEZA UBUNIFU** wa sera za kupinga ubaguzi wa rangi ili kutumiwa na watu walioathiriwa vibaya na ubaguzi wa rangi.

Tungependa kusikia maoni na mawazo yako juu ya Utafiti huu, kivipi unaweza kufanya kazi vizuri zaidi ili kutoa sera zitakazotumika kuleta mabadiliko nchini Scotland. Tafadhali SCAN QR CODE kwa kutumia simu yako ili ukamilishe utafiti wa dakika 2.




Kwa habari zaidi, unaweza kututumia barua pepe kwa: **iggantiracism@gmail.com**.